



Maswali na Majibu (jamaa)

Q. Jamaa ina jihusisha kwa njia gani?

Jamaa hubadilisha njia ambazo virusi vya ukimwi huenezwa, hii ni moja ya sababu ambayo nchi zingine ziko na nambari kubwa ya watu wenye virusi na zingine ziko na nambari ndogo. Kuna njia mingi kama vile :

1. kukataa ugonjwa wa ukimwi uko – jamaa na watu wa jamaa hiyo hukataa ya kwamba ugonjwa wa ukimwi unawadhuru .
2. Masomo – kukosa masomo ya kutosha na ujumbe wa kutosha kuhusu ugonjwa wa ukimwi huongeza nambari ya watu wenye virusi .
3. Matibabu – ukosaji wa matibabu ya kutosha ,madawa ya kutosha ya vifaa vya kupima damu pia huongeza uenezaji wa virusi kwani hakuna vifaa vya kutosha vya kupima damu.
4. Vita – Kama hakuna amani basi watu hawafuati mtindo wa kawaida na kuna kesi nyingi za ubakaji na pia ukahaba inayohusu wana majeshi ambao huwa wanaleta amani na baadaye wana majeshi hawa huenda nchi zingine na kueneza virusi hivi kwa mfano huko Rwanda na pia Congo.
5. Pia watu kuhama kutoka pande moja ya dunia hadi nyingine kama vile wakimbizi ama kwasababu ya vita , nambari ya watu wenye virusi huongozeka kwani kuna kesi za ubakaji na pia ukahaba.
6. Hali ya maisha – umaskini hufanya watu wafanye biashara hatari kama ukahaba ili kupata pesa ya karo au pesa ya kujikimu , pia wanawake hawapati masomo ya kutosha na inabidi waishi maisha ya kichini kwani hawana njia ya kujikimu.
7. Magonjwa ya zinaa – magonjwa ya zinaa huwa njia moja ya kueneza virusi vya ukimwi na kama kuna nambari kubwa ya magonjwa haya basi kuna nambari kubwa ya watu wenye virusi vya ukimwi.

Q .Sina uwezo wa kubadilisha njia hizi , hii inamaanisha sina nia?

Hapana haimanishi hivi, Njia hizi haziwezi malizwa na mtu mmoja. Vita na hali ya nchi ya maisha haziwezi malizwa na mtu mmoja na hii haimaanishi yakwamba utapata virusi vya ukimwi inamaanisha kuna uwezo mkubwa tu. Tuna paswa kubadilisha tabia zetu ili tuweze kujichunga, Pia tunapaswa kukubali ya kwamba ugonjwa w ukimwi uko na tutafute njia ya kujikinga , mtu yeyote mwenye ugonjwa wa zinaa anapaswa kutafuta matibabu kwani kuna matibabu na hii inateremsha hatari ya kupata virusi vya ukimwi. Kila siku watu 14,000 wanaambukizwa virusi vya ukimwi na tunaweza saidia teremsha nambari hii ili tuweze kuishi maisha marefu yenye afya .